# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME

**10/11/2022**

## TANGAZO LA ZABUNI
## WANANCHI WOTE

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa na uwezo kutoka ndani na nje ya Wilaya ya Tarime kwamba anakaribisha maombi kwa zabuni ya Usafi wa Mazingira katika Halmashauri kwa mwaka wa fedha **2022/2023 (DISEMBA 2022 HADI 30 JUNI 2023)**

2. **ZABUNI YA USAFI WA MAENEO KATIKA KATA ZIFUATAZO**

| | Maelezo ya kazi | Namba ya zabuni | Ada ya maombi ya zabuni Tshs |
|---|---|---|---|
| ii | 1. KATA YA MATONGO | LGA/067/2022/2023/NC/02 LOT 2 | 20,000.00 |
| iii | 2. KATA YA NYAMWAGA | LGA/067/2022/2023/NC/02 LOT 3 | 20,000.00 |

3. **SIFA NA MASHARTI YA MWOMBAJI:-**

i. Mwombaji anatakiwa kufanya utafiti kwenye eneo analotarajia kufanya usafi ambapo mzabuni atakuwa anakusanya, anazoa, atasafirisha na utupa taka katika eneo maalum
ii. Mwombaji aambatanishe kivuli cha leseni hai ya kazi ya uzoaji taka, hati ya usajili wa walipa kodi (TIN) pamoja na hati ya usajili iwapo mwombaji ni kikundi, Ushirika au Kampuni. Iwapo mwombaji ni mtu binafsi awe Raia wa Tanzania na aambatanishe barua ya utambulisho wake kutoka kwa Mwenyekiti wa Kitongoji na Kijiji pamoja na kivuli cha kitambulisho cha mkazi/ Mpiga kura
iii. Mwombaji awe na Uzoefu wa kazi aliyoomba kwa muda wa mwaka (1) katika kazi hiyo.
iv. Mwombaji awe na Uthibitisho wa ulipaji kodi (Tax clearence certificate)
v. Mwombaji asiwe mtumishi au Kiongozi katika Halmashauri ya Wilaya ya TARIME.
vi. Uthibitisho wa uwezo wake kifedha (Bank statement) kuanzia Januari 2022 hadi Juni 2022.

vii. Muombaji aambatanishe uhalali wa kisheria (Power of attorney) wa mtu atakayehusika na zabuni hii.

**viii. Awe na wafanyakazi / vibarua wa kutosha (CV), Awe na wataalaam washauri wa fedha na Afya na mazingira**

ix. Mwombaji wa zabuni anapaswa kuambatanisha dhamana ya zabuni kwa ahadi **[Bid Security Declaration]**

x. Mwombaji awasilishe mpango kazi unaoonyesha jinsi atakavyotekeleza majukumu yake katika kipindi cha makataba.

xi. Mwombaji anatakiwa alipe ada ya maombi ya **Tshs. 20,000.00** ambayo haitarudishwa. Kwa kutumia Control No. ya Halmashauri.

xii. Mwombaji atapatiwa Nyaraka za **Zabuni kutoka Ofisi ya Katibu wa Bodi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime (ofisi ya zamani Bomani) baada ya kulipa ada ya maombi TSHS. 20,000/=**

xiii. Zabuni hii ipo wazi kwa mtu binafsi, kikundi cha watu kilichosajiliwa Kisheria, Ushirika, Kampuni au Serikali ya Kijiji, ilimradi awe na sifa na uwezo wa kufanya shughuli hizi na awe tayari kuheshimu Mkataba.

xiv. Mwombaji ambatanishe katika maombi yake tamko la kutojihusisha na vitendo vya Rushwa au ushawishi wa aina yoyote, fomu ya tamko hili imeambatanishwa ukurasa wa mwisho wa kitabu cha zabuni.

## 4. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI:

i. Mwombaji awasilishe zabuni halisi na nakala mbili, endapo maelezo ya halisi na nakala yatatofautiana maelezo yaliyopo kwenye nyaraka halisi ndio yatatumika kwenye tathmini.

ii. Maombi yatumwe kwa **Katibu Bodi ya Zabuni Halmashauri ya Wilaya ya Tarime S.L.P 16 TARIME.** Juu kabisa ya Bahasha paandikwe kwa herufi kubwa **Zabuni ya usafi MFANO KATA YA KEMAMBO ZABUNI NA: LGA/067/2022-2023/NC/02 LOT 1** katika bahasha hiyo pasionyeshe alama yoyote ya utambulisho wa mwombaji juu ya bahasha pia paandikwe usifungue kabla ya saa **4.30 asubuhi.**

iii. katika bahasha hiyo pasionyeshe alama yoyote ya utambulisho wa mwombaji juu ya bahasha pia paandikwe usifungue kabla ya saa 4.30 asubuhi.

iv. Bahasha ifungwe madhubuti kwa **LAKIRI** na ndani ya bahasha iambatanishwe stakabadhi halisi ya malipo ya ada ya maombi, na vivuli vya leseni,cheti cha usajili wa kampuni ,cheti cha utambulisho wa kampuni kisheria (certificate of incorporation) na hati mbalimbali zenye kutambulisha uhalali wa mwombaji / maombi.

v. Nyaraka za maombi ya Zabuni ikiwa imeambatanishwa na barua ya maombi itumbukizwe ndani ya Sanduku la Zabuni lilipo katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji

(W) (ofisi ya Halmashauri ya zamani Bomani) **kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 9.30 mchana siku za kazi tu.** Mwombaji anapaswa kusaini katika kitabu cha kupokelea zabuni.

vi. Zabuni inadumu (Tender validity) kwa muda wa siku 30 baada ya ufunguzi.

vii. Mwombaji /mwakilishi wake anashauriwa kuhudhuria zoezi la ufunguzi litakalofanyika kuanzia saa 4.30 asubuhi katika ukumbi wa Halmashauri ya Tarime (Ofisi ya Halmashauri - Bomani).

viii. Mwisho wa kupokea maombi ni **18/11/2022** siku ya jumatatu saa 4.00 asubuhi, maombi yoyote yatakayoletwa baada ya saa 4:30 Asubuhi hayatapokelewa na ufunguzi utafanyika siku hiyo hiyo muda mfupi baadaye katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri. Halmashauri hailazimiki kukubali au kukataa zabuni yoyote ambayo haikuzingatia sheria ya manunuzi ya umma Na 7 ya 2011 na Kanuni zake GN 446 ya 2013 pamoja na marekebisho ya 2016.

ix. Maombi yaliyochelewa, ambayo hayakusomwa wakati wa ufunguzi au yaliyotumwa kwa Fax, Telex, Telegram au maombi yaliyonakilishwa hayatafikiriwa kwa namna yoyote ile.

-

Solomon I. Shati
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA TARIME**

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
TARIME DISTRICT COUNCIL